**TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) MHANDISI BENEDICT NDOMBA, KWA MHE. RIDHIWANI KIKWETE (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA SITA (6) CHA SERIKALI MTANDAO TAREHE 19 FEBRUARI, 2026 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

**Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb)*;*** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ,

**Mhe. Amos Makalla,** Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

**Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro,** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria

**Ndg. Mululi Mahendeka;** Katibu Mkuu Ikulu

***Makatibu Wakuu wote,***

***Dkt. Mussa Kisaka;*** *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Wakurugenzi*** *wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,*

***Wakuu wa Idara*** *za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali*

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo,*** *na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;*

**Viongozi wa Dini,**

**Waandishi wa Habari**,

*Itifaki imezingatiwa;*

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutuwezesha kuhitimisha salama Kikao Kazi hiki cha Sita (6) cha Serikali Mtandao kilichofanyika kwa siku tatu hapa jijini Arusha.

**Mhe. Waziri**;

Kwa dhati kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kushiriki nasi katika kuhitimisha kikao kazi cha sita cha Serikali Mtandao hii leo, kilichofanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 17 Februari katika ukumbi huu wa AICC. Tunashukuru kwa kuja na tunasema asante sana!

**Mhe. Waziri**;

Kikao Kazi hiki cha siku tatu kimewakutanisha zaidi ya wadau 1,000 wa Serikali Mtandao kutoka sekta za umma na binafsi, ambapo mada 14 zinazohusu jitihada za Serikali Mtandao zimewasilishwa na kujadiliwa kwa kina ili kuimarisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Kupitia mijadala hii, tumepata fursa ya:

- Kutathmini utekelezaji wa maazimio ya Kikao Kazi cha Tano cha Serikali Mtandao,
- Kuainisha mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini,
- Kujadili changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzitatua,
- Na kuweka maazimio mapya yatakayotuongoza katika hatua zinazofuata za kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma za umma kupitia mifumo salama na jumuishi ya Serikali Mtandao.

**Mhe. Waziri,**

Katika Kikao Kazi hiki, pamoja na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao iliyofuatiwa na mijadala mbalimbali kutoka kwa wadau, Mamlaka pia, kwa mara nyingine, imeandaa tuzo ambazo utazikabidhi baadaye kwa taasisi zilizofanya vizuri katika uzingatiaji wa **Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika Ujenzi, Uendelezaji, uendeshaji na Usimamizi wa miradi ya TEHAMA Serikalini**.

Tuzo hizi zinalenga kutambua na kuthamini jitihada za taasisi za umma zilizotekeleza miradi ya TEHAMA kwa weledi, uwajibikaji na kwa kuzingatia misingi ya Serikali Mtandao ili kuwa mfano na kutoa hamasa kwa taasisi nyingine.

**Umuhimu wa tuzo hizi ni pamoja na:**

- Kukuza utamaduni wa uzingatiaji wa sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao,
- Kuhamasisha ubunifu na ubora katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA,
- Kupunguza hatari za upotevu wa rasilimali za umma,
- Kuhamasisha taasisi nyingine kuzingatia kikamilifu sheria, kanuni, miongozo, viwango na taratibu zilizowekwa, na
- Kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inakuwa salama, endelevu, jumuishi na inayotoa thamani halisi kwa wananchi.

**Mhe. Waziri,**

Kikao Kazi hiki pia kimetumika kama jukwaa muhimu la kutafakari na kujadili **Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka 50** katika eneo la Serikali Mtandao, inayolenga kuijenga Serikali itakayokuwa ya kidijitali kikamilifu na inayotumia mifumo iliyounganishwa, salama. Lengo ni kuhakikisha kuwa katika kipindi cha muda mrefu, Serikali Mtandao inakuwa:

- Nyenzo wezeshi katika kukuza uchumi wa kidijitali,
- Nguzo ya uwazi, uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa,
- Kichocheo cha ubunifu na matumizi ya teknolojia za kisasa, na
- Msingi katika utoaji wa huduma bora, jumuishi na zinazopatikana kwa wakati,
- Kukuza vipaji na kutengeneza Ajira kwa vijana wabunifu katika eneo la serikali Mtandao.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), itaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wote wa Serikali Mtandao kuhakikisha kuwa, **Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050** inatafsiriwa katika mipango ya utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini ili kuleta tija kwa maendeleo ya Taifa letu.

**Mhe. Waziri;**

Kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), napenda kuwashukuru kwa dhati washiriki wote kwa kujitokeza kwa wingi, kushiriki kikamilifu katika mijadala na kuchangia mawazo mazuri kwa mustakabali wa maendeleo ya Serikali Mtandao. Ushiriki wenu umeonesha dhamira ya dhati ya pamoja ya kuijenga Serikali inayotumia TEHAMA kwa ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa maslahi ya wananchi.

Aidha, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Uongozi wa Mkoa wa Arusha, kwa ushirikiano mkubwa, mapokezi mazuri na kuwezesha mazingira bora ya kufanikisha kikao kazi hiki. Vilevile, tunawashukuru wadhamini wote kwa mchango wao mkubwa uliowezesha kufanyika kwa kikao hiki kwa mafanikio.

**Mhe. Waziri;**

Mamlaka inawahakikishia washiriki wote kuwa, maazimio yaliyofikiwa katika kikao kazi hiki yatafanyiwa kazi kwa karibu kwa kushirikiana na taasisi husika, ili kuhakikisha yanatekelezwa kwa wakati ili kuleta tija iliyokusudiwa. Vilevile, Mamlaka itaendelea

kutumia majukwaa kama haya kufuatilia utekelezaji wa maazimio, pamoja na kusikiliza changamoto za utekelezaji wa Serikali Mtandao ili kuimarisha ushirikiano baina ya wadau wote wa Serikali Mtandao.

Kwa heshima kubwa, napenda kumshukuru tena **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** kwa maono yake, uongozi thabiti na uwekezaji mkubwa unaofanywa kwenye sekta ya TEHAMA, ambao umeendelea kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma mtandao salama na jumuishi, hali ambayo inarahisisha kuijenga Serikali ya Kidijitali.

Asanteni sana kwa ushiriki wenu, tunawaombea msafiri salama na muwe mabalozi wazuri wa mageuzi ya kidijitali Serikalini.

**“Kwa pamoja tuijenge Serikali Mtandao”**

**Kazi na utu……………………………**

Asanteni kwa kunisikiliza.